*AAP 42 (1995): 41-72*

# HISTORICAL TEXTS FROM THE SWAHILI COAST (PART II)

DEREK NURSE

**Contents of part II:**



| | |
|---|---|
| Upper Pokomo | Asili ya Mp$^h$okomu |
| | Fumo Liongo |
| Elwana | A story |
| Mwiini | Proverbs and riddles |
| Bajuni | Mashairi |
| Pate | Saidi Haji talking about poetry |
| Amu | Kiṯeko, a story |
| | Verse by M.A. Abdulkadir |
| | Women's political songs |
| Shela | An old woman reminisces |
| Matondoni | Mbaraka Msuri, a hadithi |
| | Ngano |
| Mwani | A story |

Upper Pokomo : Asili ya Mp$^{h}$okomu (Origin of the Pokomo), recorded by M. D. J. Jarha from an elder in Kitere village

E Mp$^{h}$okomu βayaβa na Shungwaya. E maná βadaramieo na Shungwaya mpaka kuno ni
The Pokomo come from Shungwaya. The reason why they ran from Shungwaya to here is

kwamba βadarama Gaβirha na Karaji. E βant$^{h}$u βano βakiywana ne Mp$^{h}$omomu na
that they ran from Somalis and Orma. The(se) people were attacking Pokomo and

Koshoro. Duβa e Mp$^{h}$okomu ne Koshoro βadarama
Mijikenda('people who live in the wilderness'). So the Pokomo and Mijikenda ran

kuyaβa na Shungwaya ili βakajifiche bia ingini ili βaseyagwa. βakifika kuno
and left Shungwaya to hide themselves place other to be not killed. Reaching here

kwe chana ye maro e Mp$^{h}$okomu βasaa. E Koshoro βenda usoni, kwa kwamba e maisha
at river of Tana the Pokomo stayed. The Mijikenda went ahead, because the life

yao ni maisha ya badani. E chana ye maro ilikua kwe Mp$^{h}$okomu ambao e maisha
their is life of wilderness. River of Tana was good for Pokomo, whose life

yao ni maisha ya kuima. Nde mana ambao e Mp$^{h}$okomu βasaa kuno chana, ao e
their is life of farming. It is reason why Pokomo stayed here at the river, but the

Koshoro βenda usoni. Lakini e asili yao ni kwamba βobada βayaβa na bia moja.
Mijikenda went ahead. But the origin their is that all they come from one place.

Upper Pokomo : Fumo Liongo, recorded by Mr. Jarha from the same elder

Fumo Liongo alikuwa munt$^{h}$u ywa βito. Alikuwa mufalume ywa βito. E βakati avyaiyweo
Fumo Liongo was person of Witu. He was chief of Witu. The time when he was

na akitaβali haukumanyikana, mana havikuwa na kuandika e βakati ude. Fumo Liongo
born and ruled is not known, because there was no writing at that time. Fumo Liongo

alikuwa mukuyu munene na mwenye nguvu nyingi sana. Kamanya kupigana sana. Alikuwa
was huge, stout, and very strong. He knew to fight well. He was

sujaha ywa kutumia uha na nchh$^{h}$ale. Kaβa mukali mump$^{h}$aka e ma'adui βakwe βafikiri
skilled in using bow and arrows. He was fierce so that enemies his thought

kwamba nk$^{h}$anafwa kabisa, na βala nt$^{h}$avi kint$^{h}$u kya kumuyaga. Kwa hivyo e
that he will not die completely, and there is nothing to kill him. Therefore the

ma'adui βakwe βamuhuma e mwana ywa Fumo Liongo amuuze ise kwamba ni kint$^{h}$u ga
enemies his sent-him the son of Fumo Liongo to ask his father that it is thing what

kyaβeza kumuyaga. E ise karara kwamba e mwana ywakwe kahumwa na ma'adui βakwe. Kwa
can kill him. The father found that child his was sent by enemies his. There-

hivyo kamwamba e mwana ywakwe, 'Nimanya kwamba kuhumwa ili nikwambie e kint$^{h}$u
fore he told the son his , 'I know that you are sent so that I tell you the thing

kyaniaga ili uniage. Lakini hakona nifwa, ðade ðangu ðe kuzikwa aβe unazikwa
that kills me so you may kill me. But if I die, there my being buried will be where

e mbego. Ami, lilima tu yaβeza ikaniaga. Kona kuhaya lilima
you will be buried at my side. For me, needle alone can kill me. If you take needle

kisa kunitora e kikovu nanafwa mara moja'. E mwana kenda kaβambia ma'adui
then stab me the navel I will die immediately'. The son went and told enemies

kwamba e ise ayagigwa na lilima. E ma'adui βamwamba e mwana ya kwamba kona
that the father is killed by needle. The enemies told the son that if

kamuyaga ise βamuhendeza e mufalume ywao. Kwa hivyo e mwana kamureba ise akigona
he kills father they make him leader their. Therefore the son waited for father to sleep,

kahaya lilima kenda kamutora ise e kikovu. Ise akifwa e ma'adui βamugwiya e mwana
took needle went stabbed-him father navel. Father when-he-died enemies seized son

ywakwe kisa βamuyaga. βo βaβili βazikwa baɗe moja ja vide ambavyo ise kanena.
his then killed him. They two were buried one place as father had predicted.

The symbol ['] represents a glottal stop. The phonetic details of this passage are reasonably represented.

Elwana : story told by schoolboy to Norman Townsend

Eye ni mamasa ya jarsa ya wailwana ana izicho limoza. Siku moza jarsa eye apeja
This is story of old man of Elwana he has eye one Day one old man this wanted

kocha mudura. Atana moka eye wa dura, amwabya ateni, 'Uwe sasa ujarie dauwakuβiala,
to marry girl. He called wife his first told her that 'You now have aged you cannot

kwa hivyo emi nimukupejeni moka oge'. Jarti eye amwabya ateni,'Lola uwe
bear again, therefore I will marry wife other'. Old woman told him that,'Look to

mwenye'. Jarsa eye amamata kwa siku dato, siku ya nna amujibu moka weye ateni,
yourself'. Old man thought for days three, day fourth he replied to his wife that,

'Emi sasa ni mutayari kocha'. Eda a'alimia mudura. Mudura iyo amuɟaama akafai sana,
'I now am ready to marry'. He went talked to girl. Girl this liked him much very,

maana yaye jarsa eye ni tajiri (duruma). Mudura amwabya ateni, 'Emi niβiazilwe, kwa
because he old man is rich. Girl told him that , 'I am ready to be

hivyo ghaya kwa wazee wemi'. Na iyele era amuri ya mudura, aghaya kwa wazee na
married so go to parents my'. And he obeyed order of girl, he went to parents and

wamuɟaama. Jarsa eye yagalela nyubeni agheghela mele. Aola sokari, gunia lya
they liked him. Old man returned home prepared body. He bought sugar, sack of

biridha, korma ngobe, mochozi wa biridha, jiβica ngozi ya mikaha, na maghuo ya
rice , bull cow , sauce of rice , ram sheep for seventh wedding day, and

wainao. Isana alika dagha wakoza harusini waβine. Eda
clothes for mother her. Then he invited people they come to wedding to dance. He went

aherimelwa. Dagha wafurahi akafai sana. Baada ya siku tolba, ocha moka waye
was married. People rejoiced much very. After of days seven, he married wife his

agalela mozeni kwaye. Jarsa eye na mudura oyo wasiakuβiala yita farha, wazaza
returned to village his. Old man and girl this bore children many, they filled

moze. Mamasa na dieradi na gaβaβadi.
village. Story be short and long.

It is certain that phonetic details of this passage are incomplete.

Mwiini: proverbs[1]

1. Aad̲a ya mtaana maneeno, ya młungaana shteendo.
   Custom of slave(is)talk, of the free man(is)action.

2. Ad̲ui mpeend̲e.
   Love your enemy.

3. Ahd̲i ni d̲eeni ka munt'u nayo d̲iiní.
   Promise is debt for person with religion.

4. Ałama yaa nvuła ni mawiingu (also d̲ałiłi for ałama)
   Sign of rain is clouds.

5. Aaxibi ha'iwołi.
   Reserve does-not-rot.

6. Axiłi ni maałi.
   Intelligence is wealth.

7. Axiłi niingi hubasha ma'arifa.
   Much wealth loses understanding.

8. Ba'ad̲a ya diixi ni faraji. (also ba'ad̲aa for ba'ad̲a ya)
   After hardship is relief.

9. Babaa nk'aambo si baaba. (also waawa for baaba)
   Stepfather is not father.

10. Baret̲o mp'uundá hapaandi farasi.
   Person-used-to donkey does-not-mount horse.

11. Chaako chiwovu si cha muunt'u chisuura.
   Your bad (thing) is not (that) of good person.

12. Chała chimooyi hachuβli nt'awa.
   One finger does-not-kill louse.

13. Cheema huza ruuhuye chiwovu humershoowa.
Good-thing sells itself, bad-thing is-advertised.

14. Chilasila lfuooní hupatikana bahariini.
What-is-left on-shore is-found in-the-ocean.

15. Chili chaawe nt'ukichiɫaalilá hiiwi nk'ungu ize.
Your bed you-do-not-sleep-in-it you-do-not-know its-bedbugs.

16. Chiɫoho pashpo chaambo hashpati nsi. (also biɫaa for pashpo)
Hook without bait does-not-catch fish.

17. Chint'u shpia hupeen̲d̲eza hat̲t̲a shchiwa chijarahá.
New thingspleases even if it-is a wound.

18. Chiwozeɫó nt'achina lbaani. (also cha kuwoɫa for chiwozeló)
That-which-is-rotten has-not incense.

19. D̲axt̲ari hareebi ajali.
Doctor does-not-stop fate.

20. D̲awa yaa mulo nii mulo.
Remedy for fire is fire.

21. D̲ibi(i) mbiɫi haskaɫi karka moro mooyi.
Two bulls do-not-live in one enclosure.

22. Ebu ya mait̲i hiiwó mwosha mait̲i.
He-who-knows shame of body (is) washer (of the) corpse.

23. Finika shkoombe mwaachisi napite.
Cover cup (until) bastard goes-away.

24. Ha'isii kufá naɫangale qabri.
He-who-does-not-know death let-him-look-at grave.

25. Habba na habbá huyeza shkaba.
    Little and little fills small-bucket.

26. Haraka haraka nt'aina baraka.
    Hurry hurry has-not blessing.

27. Hutio mwaana kulá ndie huló. (also hulo ndié for ndie huló)
    He-who-fears (for) child (to) cry is he-who-cries.

28. Ichawakoo niá yikoo nd̲iɬa. (also huwako for yikoo)
    Where-there-is will there-is way.

29. Ina isuura huwaza n̲uumba.
    Good name brightens house.

30. Kaafiri xiinfó ni xeeri kolko islamu sho xiinfa.
    Infidel who-is-of-use-to-you is better than Muslim who is of-no-use-to-you.

31. Kamaa we chiwona chiint'u chiza kuhad̲a chiint'u haixupati chiint'u.
    If you see something, if you refuse to-say anything, you-get nothing.

32. Kaazi isho shpiimo mwiishowe huɬanya waant'u.
    Work that=has-no measure in-the-end causes-to-fight people.

33. Kiwa kuwa beɬee nd̲iɬá nd̲iyoo nd̲iɬa.
    To-know that you-have-lost the-path, that-is the-path.

34. Kula hendo iɬú kuzimu hashkomi, hishkila.
    Everything that-goes up doesnt-arrive, it-comes-down.

35. Kula mooyi huvuna yaa ye yaaziɬó.
    Each one harvests what he has-sown.

36. Limi nt'alina mwishpa.
    Tongue has-not bone.

37. Maneeno ni makałi xshinda lpaanga.
Words are sharp -er than sword.

38. Maskiini histirika kaawe, dhibuye hanza chiwa mgeeni.
Poor-man is-not-seen in-his-place, his-difficulties begin when-he-is a stranger.

39. Mato ya mwenewe humwandisha ngoombe.
Eyes of owner fatten cow.

40. Mbigaa nk'ele ha'ushi ziwovu mimbaani.
He-who-makes noise does-not-hide evils inside.

41. Mtumba ibohołi hingiłó ye mwenewe.
He-who-digs hole enters he himself.

42. Mtumba xabri mwiishowe hutumbilowaa ye.
He-who-digs grave in-the-end is-dug-for him.

43. Munt'u wa xupa koodhi hakosoowi, hapatikaní ni munt'u wa xupaa kuja.
Person to give (you) advice does-not-lack, he-who-is-not-found is person to give food.

44. Nt'ale ilaziłó hairuudi chinume.
Arrow that-has-left does-not-return back.

45. Simwoondołé ifiriti łeełó.
Don't wake giant who-sleeps.

46. Siwałaangé wanaank'uku nt'asaa wo kuwanguloowa.
Don't-count chickens before they hatch.

47. Shpowa chaała simizé chotte.
If-you-are-given finger, don't-swallow it-all.

48. Wowi asliye ni matete yaa nvuła.
River it's-origin is drops of rain.

Riddles

1. Chiiko laakini hichiwoni. 'It is there but one does not see it'.
   Lkosi. 'Nape of the neck'.

2. Chint'u chimooyi huzałoo miá. 'One thing which gives birth to a hundred'.
   Awuuri. 'The seed'.

3. T̲ała haako masku mazimá biła maft̲a na lt̲aambí. 'A lamp which burns all night without oil or wick'.
   Mwezi wa weełu. 'The moon'.

4. Hałaałi wała ha'ineendi, uko naxułangala tú. 'It doesn't sleep or walk, it is just there looking at you'.
   Piicha. 'A picture'.

5. Hujoowa huja huja hujoowa. 'It is eaten, it eats: it eats, it is eaten'
   Mp'aamp'a. 'A shark'.

6. Lkaambała nii liłe laakini halxaad̲iri xfunga skunyi. 'The rope is long, bit it cannot tie firewood'.
   Nd̲iła 'A road'.

7. Mt̲ungiini kaaka kata hayiingili. 'In my water jar a ladle does not enter'.
   Nt̲'upa. 'Bottle'.

8. Muundawa ni mkułu, laakini mavunoye hayayezi lkusi. 'My farm is big, but its harvest does not fill the hand'.
   Mashuungi. 'Hair'.

9. Nk'ukuwa taziłe miwaani. 'My hen has laid among thorns'.
   Ananaasi. 'Pineapple'.

10. Polpołoo mbiłi hugudhbat̲oo wowí. 'Two areca nuts which cross a river'.
    Maat̲o. 'Eyes'.

11. Saa'aya nt'aixsimama nt'angu itila lfuungułó. 'My watch never stopped since it was wound up'.
    Mooyo (or, qalbi) 'The heart'.

12. Si humkasa laakini hachimwoni. 'We hear him but we do not see him'
    Soot̲i. 'The voice'.

Mashairi

1. Nina mahala napenda
Mapendi anikechele[1]
Nami nina nipendwapo
Ambapo nipatukile
Pene raha na upepo
Ni Mayi angava tele[2]
Nenda kurai nongole[3]
Hata nende nipendwapo.

2. Hapa ndipo hapa sipo
Hoo si unahudha[4]
Ni mashuu akambani[5]
Na mikondo na chongodha[6]
Hapo huteka rubani
Asokayisi hupwedha[7]
Nchia nanga kwa widha[8]
Hayisi uielepo[9].

3. Mdhingadhinga huk'ucha[10]
Na mwenenda hukuvaa[11]
Mla cha mwendiwe
Na chake huliwa
Mtumaini cha nduu
Hufa hali masikini.

4. Mwana atoka hondeni[12]
Zhito halishi kuenga[13]
Honde ichendele yani
Haibikiki mfunda[14]
Na hii ni Ramadhani
Nasi chwataka kufunga
Shauri gani malenga
Honde hii hulimaye ?

5. Abawa[15] nalikwambia
Simtukue Akheri
Akheri mwana kijana
Haiyayua bahari
Hili lalijaliwa
La kudhikwa Dingibari[16]
Aivao[17] ni Maruri[18]
Inahadaa dunia.

6. Yapokuva alituna
Kupacha ingi[19] leusi
Ukanenda hoko hoko
Kharamu halinitosi[20]
Mwanafundi wa vangina[21]
Imekudara teveshi[22]
Na mfupa wa kavashi[23]
Hunipa mayavuyavu[24].

7. Nachive[25] havana t'ume
Vanyeme hulisa wimbi[26]
K'amwambia si mfume
Hoyo mwana wa ingi[19]
Lakini si mfalume
Wachepeu[27] na firimbi
Huyo si nachi ni dhambi
Musiudhike[28] nduyangu.

1. Anikechele = St. Sw. yamenijaa. 2. 'And although the water comes in'. 3. Nongole < -ongoa. 4. St. Sw. nahodha. 5. Ishuu 'wave': akamba 'seaweeds'. 6. Chongodha 'narrow channel'. 7. 'He who doesn't know runs aground'. 8. Widha = modern Bajuni kidha 'darkness'. 9. Uielepo 'where he slept'. 10. Huk'ucha 'gets trouble'. 11. -kuvaa = St. Sw. -kwaa. 12. Honde = St. Sw. konde. 13. Zh represents the voiced palato-alveolar fricative [ʒ]. 14. -bika mfunda 'draw a line'. 15. Abawa '(older) brother'. 16. Dingibari 'Zanzibar'. 17. Aivao 'he who knows'. 18. Maruri 'God'. 19. Ingi 'egg'. 20. -tosa = St. Sw. -tosha. 21. vangina = St. Sw. wengine. 22. Teveshi 'sinew(s)'. 23. Kavashi 'rib(s)'. 24. Iyavuyavu 'lung'. 25. Nachive = nachi valee 'those buffaloes'. 26. -nyeme < -nyama = St. Sw. -inama. 27. Chepeu 'helmet, hat'. 28. -udhika 'get angry'.

Pate : transcript of Saidi Haji talking about poetry

Nikunena kuwa dhiko lugha huchumia kwa dhiada, dhiada maana neno kuwa umelinena na limekwisa kuelea lakini mbee yake ikachumika harufu ambao kwamba haihitajiki, lakini kwa nanna ya kuimba ikawa ni ladhima ile harufu ingie. Na sharia yenyewe ya kuchumia dhiada ni kama hilo: huyu bwana alinena kwa kuwa nalina nnda Ngodhini, na Ngodhini ni kana mahala, kunena Shela, Kitau, ndio ni mahala maalumu lakini ule nnda ni mahala palipokuwa na shamba, na shamba lile likamalidhika, hakuna tena, michi yake imeondoka. Basi palee mahala paichwa ni nnda, nina nnda wangu Kitau. Basi hoo bwana anena:

Na nna nnda Ngodhini ule muuyao,
P'eche kacha ishirini na ndidhi dhipunguao,
Nami na ndemwa na deni na nke ataka nguo,

dhiada, hio dhiada huchumika ni dhiada maana kachika nguo,

Nionyana yachendwao nami nipache nichende

utakwisa kufahamu yale maneno amenena ni shairi lakini dhile harufu nngine alomalidhia kwa mwiso, hakumalidha kwa kuwa ni ladhima achumie lakini imekuwa ni ladhima achumie kwa kutegemea lile shairi kwa dhile harufu dhilale mahala pamoya. Kisa akanena, karegee mwenye kujibu, kajibiwa kuwa:

Karegee Ngodhi Mbambe unike lako iungo (ni Kisiu, Kipate, uinike lako ungo)
Mpigwa nat'i na embe hunuk'a na lake kongo,
Nke nrai mpen<u>d</u>e kwa kweli na kwa urongo,
Deni ongedha kiwango mwenye deni nakulinde,

Hidho ndidho harufu ambadho kwamba dhatokea kwa kiswahili cha dhamani, haya ni mashairi ambao kwamba yana nyaka nyingi sana. Kwa nina nch'u mmoya alikuwa hoyo ni nch'u ni nshairi na una mwenzake ni nshairi na wao hupen<u>d</u>a kugonganagongana wakati nngine mashairi. Basi kwa kule kuchiana wasi wasi ikawa hukimbianakimbiana, basi siku moya akatoka ule nshairi mmoya akenda kumwangalia ule bwana na kumwaga safari, chenda ule bwana mwenye kuagwa kimuona ule uyao basi aliisita kachika ntambuu. Ule bwana alimwona ule nch'u ameisita akaya akamwicha: bwana ee bwana ee. Ule akanyamadha asijibishe cho chot'e, ule alipokwenda kule endako akaan<u>d</u>ika shairi, kumwechea ule shaha mwenyewe alokuwa akiimba. Akamwan<u>d</u>ikia:

Wangu nsuo wa Gomo hela nichika labeka,
Mwan<u>d</u>oni kuna shokomo labuda chombo hondoka,
T'akupa ngidhi kipimo na t'umbako ya kunuk'a,
Tukua wangu waraka nipekea ban<u>d</u>arini,

Iwo chukinena, itakuwa aliponena kwa kuwa 'wangu nsuo wa Gomo', ule Gomo ni nch'u wa bara ni Mboni, 'nichika labeka, mwandoni kuna shokomo', shokomo hio nlugha huchumika Siu, shokomo ni vunda la maneno, hooo hoo hoo ho, 'Mwandoni kuna shokomo labuda chombo hondoka, t'akupa ngidhi kipimo', kipimo chalikuwa ni mfucha mmoya na nusu, itaankuliwa kipimo, 'T'akupa ngidhi kipimo na t'umbako ya kunuk'a, tukua wangu waraka nipekea bandarini'. Haya, 'Uchenenda mpe Bala', Bala alikuwa ni nahudha wa kuvusha wach'u wa bara wakiya kisiwani,

Uchenenda mpe Bala swahibu wangu autwai,
Kampe Shekhe Dumila na Muhammadi Ali,
Na Sharifu Andala na baki ya Ulamai,
Kunyamaa haifai na chuengeni dhamani('Chuengeni' ni Kisiu, Kipate 'Chwangalieni')
Na chuengeni dhamani dha kudha nyunga na nywishwa( kudha, maanake kudhanya)
Pisie ntambuuni mbwene Haji akinosha( mbwene, maanake nimwene)
Na kichapa nkononi kama nalionchusha,
Ikashabu la ipisha Haji hakunip'a nami,

Ule bwana alikuweko ntambuunu alikinoshea ntambuu kiuchia mai. Sasa ule bwana 'alionchusha ikashabu la ipisha, Haji hakunip'a nami'. Ikashabu ni hili, la ipisha ni hili ambalo kwamba nusu liko biti nusu limepishika, basi hili ndilo 'ikashabu la ipisha Haji hakunip'a nami', licha kunip'a tambuu hata kashabu limedhowaka nusu, nusu limebakia, 'hakunip'a nami' ndio huja alokimbilia akangia ndani ya ntambuu kwa sababu nisintahajie tambuu.

Ikashabu la ipisha Haji hakunip'a nami,
Nataka mudirikane musapo kuswaliisha,
Maneno haya munene mwenyenkuu Nabasha,
<u>Akiri</u> au akane ama anene lakasha,
Ikashabu la ipisha Haji hakunip'a nami,

Lakasha ni nchocho, ak'eti hapa na hapa na hapa, wach'u sita saba kudhunguka, wachocho wa chuoni, wa skuli, kisa baadae wot'e wakaangalia yuu, kainuka mmoya kadhunguka na k'ichu kaeka nyuma ya maungo kadhunguka tena raundi na ule nkono akasita, ukichunda kofia ukiichunda ile kofia utainuka wewe umfukudhe, umpije, umpijapo takwambia lakasha, basi ndio maana kama nsamehe, ni lugha ya dhijana hio ambayo kwamba wachumiao, nisamehe, basi hapijwi tena,kaa kainuka ule amedhookocha k'ofia, kadhunguka siri siri, kisa katupa kenenda hokoo aikya akiishika hukupija, kikupija mwambie lakasha au umeiona wewe ? Wewe inuka ukamwandama yeye alikuwa usimeme, ukampija akakwambia lakasha, kana kunena nimetubu, ndio maana ya lakasha.

Akiri au akane ama anene lakasha,
Ikashabu la ipisha, merejea hapo hapo, Haji hakunip'a nami,

sababu yake alikimbia, hio ndio nadhamu ch'ocho ambao kwamba chumedhoinena.

Amu: 'Kiteko', recorded by Abdulla Yusuf Makwega

Maliki Dekshelin mfalme wa Furusia alikuwa siku moya baraza kuusana walikutanika mawaziri wot'e tisia wamevaa nguo nzuri rasmi wakangia nyumba ya mitingi ya kidola na raia walo watukufu wa ilimu na siasa na matajiri takariban wat'u hamsu mia walongia katika nyumba ya palament kuhandisi ulimwengu. Na kilindo askari wamezunguka nde kwa sababu maliki uko ndani. Na mlangoni wakungilia ndani wasimeme askari k'umi zamu. Maliki kasimama kueleza khabari mambo yatakaokuwa na yasotakakuwa kupitishwa katika dola. Kitambo katiti kuna askari mmoya alipija kiteko kaa..kaa.. kaa..kateka sana, kiteko cha yowe. Walizunguka wat'u wot'e wakamwangalia alieteka. Maliki aliwaamrisha askari kwa kufanya ghadhabu k'uu mtieni pingu huyo aloteka ambae kwamba askari asokuwa na adabu kuteka mbee za wat'u wakuu, kiteko kama hicho ametuharibia akili zetu katika fikra. Hoyo asokuwa na adabu natiwe jela kashikwa kapekwa jela kafanyiwa k'esi kutiwa adabu kuusana baada ya muda wa siku t'atu. Walitoka walee wat'u wot'e wakenda zao, ile mitingi ikaharibika kwa sababu ya zile handasa akili zimezunguka hazikuwa baridi tena zimekuwa moto kwa sababu fujo la kiteko na wakazungumwa katiti watafanya siku ingine mtingi. Muda wa siku t'atu alipekwa k'oti ule askari aloteka. Wamehudhuria askari miteni wa hamsini kusikiza k'esi ya jamaa yao itak'atika namna gani, tahukumiwa kutiwa adabu gani. Maliki kawambia mawaziri wake watatu, muhukumuni hoyo asokuwa na adabu na ufalume. Waziri wa kwanda alinena, huyu adabu yake ni kuuawa. Waziri wa pili kampinga akambia, la, haikukhusu kiteko kuwa ni adabu ya kifo. Sio adabu ya kiteko kifo, la, siwa. Mt'u kuuawa kwa sababu ya kiteko akanena, huyu waziri wa pili alimpinga ule wa kwanda akanena madola yatamlaumu ufalume wetu wakanena Maliki Dekshelin memuua askari wake kwa sababu ya kuteka itakuwa hatuna hukumu ya siasa sawasawa. Haikuwa ni sawa adabu hini yataka hoyo waziri akamwambia waziri, yataka adabu yake afungwe miaka k'umi jela. Hini ni adabu k'uu. Waziri wa tatu kampinga, akamwambia twende, si mezani ya kiteko adabu ya kufungwa maka k'umi, la, haikuwa ni adabu, hio ni adabu ya aloutawala kufungwa maka k'umi. Si adabu ya kiteko ya kuuawa wala kufungwa maka k'umi. Adabu yake ni kuatishwa kazi katolewa mui, bora kuliko kuuawa, bora kuliko kufungwa. Twabibu k'uu wa Maliki walikuwepo kampinga waziri wa t'atu, uko mbee ya maliki ulee twabibu na mawaziri, ulee twabibu ni mkuu sana wa Maliki, alimzungukia Maliki huyu twabibu kamwuliza ya twabibu ni adabu gani ya kutiwa pingu katika sababu zalonenwa, sababu t'atu. Huyu amempinga waziri wa kwanda, huyu waziri wa pili amepingwa na waziri wa t'atu, sasa katika adabu t'atu hizi, tumkia adabu gani mt'u huyu ? Twabibu akamwambia, Maliki, sababu zot'e t'atu si sawa, zina makosa k'esi za mawaziri wako, kwa sababu makosa yake mt'u huyu mekukosa wewe mfalume. Haifai k'esi

kuifanya wewe, kufanywa hukumu yake na dola ingine. Huyu mfalme wa dola ingine au waziri wa dola ingine akaifanya k'esi hii kwa sababu makosa alikukosa wewe, hufanywa na dola ingine huifanyi wewe hufanywa hukumu yake na dola ingine, ni makosa kuifanya wewe mwenye hukumu. Huyu mwenye hukumu kamuhkukmu mfalme wa mui nngine au waziri. Kahukumiwa mt'u huyu k'esi itakaokuk'ata ulee mfalme mngine ndio sawa, yoyot'e takakuik'ata. Sasa wewe ukifanya wewe hukumu hii nae mekukosa wewe sio kidola. Maliki alikubali maneno ya twabibu ni sawa na mawaziri woloifanya k'esi walikubali sawa kuliko kuifanya sisi, ni sawa kuifanya mt'u nngine, mfalme wa dola ngine kwaliko kuifanya sisi, maneno ya twabibu ni sawa yalofungwa k'esi. Muda kuya waziri wa dola ngine. Maliki aliandika barua kamwita waziri mkuu wa Maliki Turki. Alipoipata barua waziri mkuu wa Maliki Turki mfalme wake akamwambia rosta[1] kwenda ziara ya siku t'ano kwenda Furusia kwa yambo aliloankuliwa Maliki kumsikiza. Alopongia ufuetene na wat'u watano waandamizi wake waziri nyuma yake wat'u watano katika watoto wake si wakubwa kumpeka katika mui wa Turki, na askari k'umi, mbee watano nyuma watano. Aliposikilia langoni wa kamlihaki mawaziri wane wa mfalme Dekshelin kumkaribisha nyumba ya Maliki, kangia katika nyumba ya Maliki Dekshelin wakaonana na Maliki wakazungumza mazungumzo mazuri kula na kunwa zakula zizuri na malazi mazuri mpaka siku ya k'esi. Siku ya k'esi wakenda katika hukumu Maliki kamwuliza waziri mukhalifu mfalme Maliki akamwambia waziri, askari wangu mshika lango tuk'atika mitingi ya kidola alipija kiteko kikubwa kateka wakashutuka wat'u wot'e ikawa twalokiyawaza yameharibika zile akili tukavunda mitingi kuifanya siku ngine. Kwa kukosa adabu kwake askari mshika lango mawaziri watatu nikawalazimisha kumfanyia k'esi ya kumtia adabu ilipofanywa k'esi isiwe nikamwuliza twabibu wangu k'esi hii ni sawa na nyani ? ya mt'u wa kwanda au wa pili au wa tatu ? akanambia yot'e si sawa kwani hukumu hii hufanywa na dola ingine haifanywi na wewe, huyu mt'u mekukosa wewe, mfalme mwingine au waziri au jaje[2] akamuhukumu atakalokwisa yeye ule hakimu wa dola ngine basi. Mawaziri watatu kula mmoya alitoa hukumu mbalimbali, mmoya alinena yapasa kuuawa, mmoya alinena haipasi kuuawa hupasa kufungwa, wa tatu kanena haipasi kufungwa hupasa kuvua nguo kutolewa mui asiye tena hapa. Ikawa akili zetu zimezunguka hawaisi yani t'atu hizi tuzifanye namna gani, mpaka nalipomuuliza twabibu ndipo aliponambia yafaa kufanya k'esi ndio nimekuamkua wewe sababu uifanye k'esi hii. Waziri wa Turki muhandisina alizitaka hukumu zalochukumiwa na mawaziri watatu kapekwa kuzisoma ya kwanda, kaisoma ya pili, kaisoma ya tatu, kazisoma kaona kweli si sawa hukumu zao, si sawa hukumu za mt'u aloteka, mukhalifu katiwa kirimbani wamehudhuria wat'u wot'e walohudhuria mara ya kwanda walipofanya k'esi

mawaziri wamehudhuria zaidi alipokuwa ulee waziri mpia. Kamwuliza mukhalifu kamwuliza ulee askari aloteka sababu gani wewe nalokupa kuteka katika mbee za hadhra za wat'u kukosa adabu sababu gani ? Walee hawakumwuliza sababu, walee walik'ata k'esi tu, huyu mbwa kuuawa huyu mbwa kufungwa, ulee sasa kamwuliza muyuzi sana wa k'esi, muhandisi. Kamwuliza mukhalifu, sababu gani wewe lolokupa kuteka, mukhalifu kamwambia, sababu ya kuzoea, sababu ya mazoea : lelozoealo ndilo ufialo. Kamwambia waziri ulee mukhalifu, mimi nimezoea kuteka sana pahali popot'e sababu lile uzoealo ndilo ufialo. Waziri kamwuliza, kwa istishhadi gani ? kwa ule uzoealo ndilo ufialo ? Kamwambia kwa istishhadi ya ngamia na p'unda na mwanaadamu kaifadhalika yalikuwa iye, p'unda na ngamia na mwanaadamu ? Akamwambia, p'unda na ngamia walikuweko kwa bwana wao, ulee ngamia kamwambia p'unda, kamwambia tukimbia huyu bwana wetu mbakhili ni bakhili chakula hatushibi tutakwenda zetu mwituni tutakula hoko tutashiba na hatatuona tena. Usiku wakavunda zizi wakakimbia kenda zao mbali hoko wakaisita. Basi walingia ndani ya mwitu wao hawaonekani, kiza, hula tu wao, kamwambia p'unda meona mambo haya, akamwambia, p'unda usilie, usilie, bwanetu takuwa hutuzengea ukilia atayua tuko hapa takuya kutushika, mimi sendi itakwenda nyama yangu, mimi sendi mpaka kufa papa hapa, na nyama yangu utatukua wewe uipeke muini. Akambia, silii, basi akak'eti mpaka siku ya pili hawezi kuizuia p'unda, amesahau, oh, oh, oh, oh, oh, ule bwana kambia, eh wako palee, kenda bwana ulee na wat'u watatu wane wako hoko wameisita wakashikwa. Waliposhikwa ngamia hataki kwenda. Kisa kumpija hataki kwenda kamtinda basi nyama katukua ulee, p'unda katukua nyama katukua hata kavundika kiuno kwa uzito ulee asiweze kwenda kanena kweli lelozoealo ndilo ufialo. Akambia, basi waziri, kwa sababu ya istishhadi hii, ilee yambo lozoea huwezi kuiziwia. Waziri, hukumu aliwauliza mawaziri, aliwauliza, fani za ziteko watekazo wat'u ni fani ngapi ? Wakanena, hatuziyui, twayua sisi kiteko kimoya tu, yaani kiteko ni furaha tu, na kilio ni msiba. Hatuyui, fani zoziteko. Waliporudi hukumu katika waziri hakimu aliwambia ziteko ni fani tisia. Kuna kiteko cha tabia, binaadamu huteka tu, pasina mahali pa kiteko yeye atateka kwenye kiteko atateka, hii ndesturi. Kuna kiteko cha siasa yaani mt'u hana tabia ya kiteko lakini wakati wa siasa yake ya yambo huteka. Kuna kiteko cha muinga, mt'u mzima huteka tu, ukimwambia neno zuri tateka tu, ukimwambia baya yeye tateka yaani yeye kama mt'u mwenye wazimu, huteka tu. Kuna kiteko cha mnafiki , utaka yambo kwa wat'u kawa yeye huiteshatesha. Kuna kiteko cha stihizai, mt'u mwenye kiburi, huteka tu wat'u. Kuna kiteko cha zihaka, mt'u apenda kufanyia wat'u zihaka na kuwatekesha. Na mwiso kuna kiteko cha mwenda wazimu, huteka tu yeye. Huyu

mukhalifu aloteka kiteko alichoteka ni kiteko cha ufani gani ? Najawabu, hatuyui. Waloinama mawaziri kit'u chao hatuyui ni kiteko cha ufani gani ? Kawambia, huyu nik'atika mt'u muinga, hamfahamu mt'u mkuu hamfahamu mt'u mdogo, pahali alipo palee hafahamu pahali gani, na kulee kwa yeye amezoea, huteka tu. Sasa mimi k'ata hukumu: mt'u huyu nasiwekwe tena mahali penye wat'u, napawe kazi ngine, kazi ya mlangoni, katika palamenti penye wat'u, na hana makosa kwa sababu ya twabia yake na uyinga mwingi, basi nimemsamehe, dismiss k'esi.

1. Rosta < English roster. There are several other Anglicisms in the text, e.g. palament(i), mitingi, dismiss k'esi, etc: 'parliament, meeting, dismiss case' etc. 2. Jaje < English judge.

<u>Verse composed by M. A. Abdulkadir ('Mau') on the occasion of a boat disaster at Shela on Tuesday, July 24, 1979.</u>

1. Yailahi ya karimu
Mwenye ezi ya kudumu
Upitishao kalamu
Kwandika yambo likawa.

2. Yailahi sub'hana
Uso mke wala mwana
Lolot'e ukilinena
Huwa pasi kuchelewa.

3. Yailahi ya mannani
Mola uso nakifani
Wambiapo yambo kuni
Hali inui khatua.

4. Ndiwe muumba kadari
Yakheri na yaloshari
Niwajibu tuyakiri
Twandame majaaliwa.

5. Hatuhili wala hili
Upitishalo jalali
Sisi mbwakulikubali[1]
Tukaridhika moliwa.

6. Hakuna mwenye uweza
Upendalo kusiwiza
Ndiwe muondoa kiza
Rabi kwa kueta yua.

7. Lolot'e likitupata
Ni lazima kufuata
Tena pasina kusita
Wala kufurisha p'ua.

8. Twaamini kwa yakini
Akhira na duniani
Insi hata majini
Wot'e mbwakuamriwa.

9. Wot'e hutwii amri
Yako ilahi jabari
Ulo na nguvu kahari
Za kuhui na kuua.

10. Tumeamini kwa dhati
Lolot'e hali tupati
Tulo hai na mayiti
Illa kwa kukadiriwa.

11. Na sisi tumesalimu
Amri kwako rahimu
Wala hatukulamu
Kwa haya yamezokuwa.

12. Tumewakosa ghafula
Wat'u wengi kwa jumla
Kwa amri yako mola
Utwekao na kutua.

13.Ndimi zetu kutamka
Kuyanena yalotukua
Hazitoeza hakika
Kwa namna yalikuwa.

14. Ni mambo mazito sana
Amri kwako rahimu
Wala hatukulamu
Kwa haya yamezokuwa.

15.Yalo ndani ya mitima
Hututeketeza nyama
Ndio haya k'aatama
Asa yakapungua.

16.Ni mambo sana mazito
Huwasha hushinda moto
Siwa k'ubwa siwa t'oto
Kwa wot'e ni sawasawa.

17. Ni kilio kilokwamba
Kikaenea majumba
Hakuna ambao kwamba
Mmoya kilo mvua.

18.Kimetutanganya sut'e
Pasi kutenga yoyot'e
Lahaula na tuete[2]
Tumshukuru moliwa.

19.Hili si langu si lako
Ndetu sut'e sikitiko
Cha mui kibaba iko
Na wangine huzidiwa.

20. Mt'u mezokosa mke
Huenga[3] zijana zake
Kiwaza mwendani wake
Wa pili aliokuwa.

21.Hangalia mayatima
Wanuna[4] waso na mama
Kisongonyeka mtima
Mato matozi kitoa.

22.Mama alokosa mwana
Alokimpenda sana
Dharabu mno huona
Zakushindwa kutukua.

23. Walokosa akhawati
Huzuni haziwawati
Kula muda na wakati
Mswiba huwasumbua.

24.Marafiki walokosa
Jaraha halitoisa
Takuwa huanda sasa
Kikumbuka yalokuwa.

25.Walokosa majirani
Watakuwa hali gani ?
Wakikumbuka hisani
Na mambo yalozoea.

26. Nao waliotanganya
Wake zao na zijana
Wangine wakiwaona
Nyoyoni huliangoa.

27.Na wat'u mui mzima
Huzuni hazitokoma
Watakumbuka daima
Kula wakihadithiwa.

28.Milele yatasalia
Haya yamezotokea
Nyaka toka nyaka ngia
Kweleza wasiozawa.

29. Kwandika mangi siwezi
Kwa kunizidi simazi
Hutetateta matozi
Mato siwezi kuvua.

30.Kab'la siyamaliza
Naomba mola muweza
Atujazi njema jaza
Na khaswa walofiliwa.

31.Tupe nyoyo za subira
Tupate malipwa bora
Tusitanganye khasara
Yafunguni kutolewa.

32. Fungu la wanosubiri
Wapatapo maathuri
Kama haya yalojiri
Zipendi kuondolewa.

33.Utupe nguvu jalali
Tuweze kutahamali
Mswiba hunu[5] thakili
Nyoyo umezoatua.

34.Yailahi ya mannani
Tupe nyoyo za amani
Tusingie makosani
Kwa mambo kuyapotoa.

35. Nao wot'e mar'humu
Warahamu yarahimu
Kwenye janati naimu
Wafuze ndani kutua.

36.Wanali na kusuudi
Taraja[6] za mashahidi
Wawe nae muhamadi
Kipendi chetu rasua.

37.Maini walogeriki
Mewatukuza khalaki
Kwa kuwapacheo hiki
Kikubwa cha kuzengewa[7].

38.Hakuna la kuwaswibu
Kabisa lenye taabu
Kwa uwezo wa wahabu
Dhambi wameghufiriwa.

39.Rabi mewapa taraja
Waitamanio waja
Na kwetu sut'e ni haja
Taraja hio kupoa.

40.Mola amewakhitari
Kuwavika lenye nuri
Koja lao ab'rari
Wat'u waloteuliwa.

41.Hili nalituliwaze
Na nyoyo litupumbaze
Kwa kuyua tarajaze
Wao walotunikiwa.

42.Natusituse mipaka
Katika kuhuzunika
Tuk'eti tukikumbuka
Mambo yamekadiriwa.

43.Nimekoma wasalamu
Naimaliza nudhumu
Kwa kumuomba karimu
Atupe yake afua.

44.Tuafu rabi tuafu
Utwepulie machafu
Nakula ya uvundifu
Ndiwe mwenye kuyepuka.

45.Ulotupija kibati
Kwa makosa twalohiti
Yailahi jabaruti
Taababi tumekuwa.

46.Ya rabi haya mateso
Yawe basi ndio mwiso
Zingarishe zetu nyuso
Na nyoyo kuzikatua.

47.Twepulie kula dhiki
Tulizo nazo khalaki
Tupe k'undufu riziki
Matata kuyatatua.

48.Twepulie kula baa
Utupe ya manufaa
Na hiki kizaazaa
Ukikomeshe moliwa.

49.Rabi situonde tena
Kwa haya tumezoona
Kwani ni mazito sana
Na sut'e tumeemewa.

50.Ya rabi iwe ni basi
Mola turahamu nasi
Ziwa swiike nafusi
Na mswiba kuyondoa.

51.Rabi yatie kikomo
Yafusie kwenye shimo
Yasalie momo homo
Miini kutoetewa.

52.Rabi mola yamalize
Mazito usitwengeze
Na haya utueleze
Kuweza kuyatukua.

53.Ya rabi zakoneema
Utuete daima
Utwepulie nakama
Zisitubakie toa.

54.Tuswafishe tuswafike
Waume na wanawake
Amrizo tuzishike
Zot'e tuloamriwa.

55.Ya rabi tupe auni
Tushikamane na dini
Na kumshinda shetwani
Na kula mla aniwa.

56.Amina rabi amina
Tuafikie rabana
Haya tumezoyanena
Kabuli kupitishiwa.

57.Na mt'u alonudhunu
Ni Mahmudu isimu
Makazi ni hapa Amu
Na ndiko nilipozawa.

1. Mbwakulikubali = ni wa kulikubali 'we have to agree to it'. 2. -eta 'bring'. 3. -enga 'look at'. 4. Mnuna 'younger sibling'. 5. Hunu 'this'. 6. Taraja 'bridge'. 7. -zengea 'look for'.

Womens' political songs from an election in the 1970's

1. Aloufisidi mui
Mola memrufaisha[1]
Mbwafanya mbwai mbwai[2]
Magofu kutobakisha
Akifumiwa na mai
Asipate pa kwegesha.

2. Bwana una kite[3]
Hupita kilia
Hawa k'uku wake
Wamemkimbia
Ndio mwaka wake
wa kuvundika.

3. Tulipok'ata shauri
Sisi wanyonge[4]
Hela hawa mabepari
Natuwapije
Waateni waipare[5]
Wana uwambe[6].

4. Yale makoti manene
Yameanguka t'iati[7]
Walimwengu ni wageni
Ushile[8] wakati wenu
Yeo chanda tuwaonye[9]
Twalowapiga ni hiki.

5. **Zit'u zot'e tumezanya**[10]
Tunapo tushishiepo[11]
Na mola wetu Rabana
Uko nasi hapo hapo
Mambo yana wenu Bwana
Aliyoshika upepo.

6. Wende kitaruni[12]
Kwa padiri wao
Kufanya hesabu
Ya hasara yao
Wapiziwe lana[13]
Kwa umoya wao.

7. Mwalikitumia khila
Na urongo mukiapa
Sasa hamba[14] lahaula
Na mumekuwa hutada[15]
Pesa zenu tumekula
Na voti hatukuwapa.

Mwalitukua khatua
Ya kutatia tandini[16]
Tandi mwalitandua
Tukawawika shingoni
Kadi mlizonunua
Zilikuwa za barani.

8. Fungani zenu siasa
Na yot'e mulokidai
Hiki kiti mumekosa
Komeshani udarai
Ubepari umekwisha
Na mapesa hayafai.

9. Yeo natupije p'embe[17]
Vugo tukishangilia
Tuwapije kwa ziyembe[18]
Wakari wasio na haya
Waipare kwa uwambe
Ukungu ukiwenea.

1. -rufaisha 'chase away'. 2. 'He has made him like a wild dog'. 3. Kite 'pain'. 4. -nyonge 'weak'. 5. 'Let them scratch themselves'. 6. Uwambe = wambe 'dust'. 7. T'iati 'earth, soil'. 8. Ushile 'it has finished'. 9. -onya chanda 'point at'. 10. Zit'u 'things'; -zanya 'sell'. 11. =shishie = St. St. -meshika. 12. Wende(e) kitaruni 'they have gone to the enclosed space (= palace ?)'. 13. -apiza la(a)na 'curse'. 14. -amba 'say'. 15. -tada 'be rude'. 16. Tandi 'trap'. 17. Refers to beating of buffalo horns in Vugo dance. 18. Ziyembe 'razors'.

Shela : tape recording of an old woman reminiscing

Naliolewa na mt'u wa Amu, mfalme wa Amu, kaziwia washela kujenga nyumba za mawe. Alikuwa ulee ndiye mfalme wa Amu, kisa katawali muingereza, basi kapija marufuku washela hawana ruhusa kujenga nyumba za mawe. Aliko babangu, bibiye babangu alikuwa ni mwarabu na majahazi yao, tajiri hoko ikawa majahazi huk'eti hapa na mangine yako hoko, hueta mali ya hoko naye akitoa ya hapa akipeka hoko. Basi akisikia maneno yalee kawaambia wat'u wake, jengani nyumba, jahazi zimekuya, akenda kawaambia walee wat'u wa jahazini, mimi nimekuya kuwapa ripoti wat'u wa Amu wayao kutupija, hatuna ruhusa ya kujenga, kama sisi ambao ni watmuwa nasi si watumwa wa mt'u. Basi nataka waarabu wot'e mwenye p'anga aye, mwenye kisu aye, mwenye bunduki aye, wanisaidie zita. Basi wakashuka walee waarabu jahazini wakaya wakenda kulee mlima wa Hidabu walee kulee wakisikia wakarudi ndiani wakanena hakwendeki wakakimbia wakenda zao. Basi kukajengwa tena hawakusubutu tena kuya hata kisa katawali muingereza waarabu wenyewe wakashtahiana wakamtawalisha muingereza naye muingereza akak'eti na waarabu kwa uzuri akawa kama nduu. Sasa kukingia zita za muingereza, ilee milima kulee, minara ilee ilikuwa meupe, askari wakaya wakak'eti hoko kiya na wangine minazini wakaya wat'u wangi sana wakaya ni kupijana, lakini hapa wangi kukendewa kulee ng'ambo kuna minara ikabadilishwa rangi, ili jarumani akiya aone siko huku na ilee ufuoni ikapakwa rangi nyingine ili pia kuhadaa, basi kukashuka wat'u wakapakiwa wakanenda hoko Nairobi. Lakini wakisikilia hapo wenyewe waarabu zisimo kula mt'u huomba mngu lilee lilee wakisikilia kulee jarumani k'atia bendera ya amani, wataka amani kwa muingereza. Basi wat'u wakarudi wakaya zao lakini wat'u walisumbuka sana wangine walitoka mui wakenda ng'ambo kulee Manda wakenda wakaisita wangine hao waloshikwa wakatunda...uko mti wakavunda wakawatia matoni wakawa t'ongo ili wasende zitani likawa fujo kubwa sana. Hayo mimi ndio niliyoyaona.

Question: Na alikuwa wat'u wa T'akwa wakagura kulee wakaya hapa ?

Walivundika tu, hakuna sababu ya zit'u, ni wao wenyewe wakishaona hawaiwezi tena. Tukaguria hapa, ee, wangine wakak'eti kulee ndipo palipokuwa na ng'ombe kulee na mambo yot'e wakawa huk'eti kulee.

Question: Kwa nini wat'u wa T'akwa wakaguria hapa ?

Walikuwa wa papa hapa, nusu wakik'eti hapa, nusu wakik'eti kulee. Kulee alikuweko shekhe mkuu, shekhe hoyo alikuya kwa jahazi kazama kak'eti baharini t'umbi za siku kisa kaya hapa kaoa hapa Shela kazaa na mwana kaguria hoko ndio hoo ankuliwa Shekhe Kimansuri, kaguria hoko alizama, akisa kupata fahamu kipevuka taka kusafiri kwenda zake. Wat'u wa mui Shela wakamwambia, bwana huna pakwenda ina wakamwambia, bwana kaa, utakaa papa hapa, basi kak'eti kaoa kazaa na wana kabuni ulee shekhe kak'eti kulee T'akwa, kajenga msikiti na ziara yake koko hoko, wat'u hwenenda kiwa mt'u mepata yambo hwenenda kana nadhiri.

Question: Ilee ziara k'ubwa kulee ndiyo ?
Ali na karamu mwanangu. Marahamu Salima wa Shee kina mamake Ali wa Akida huyu twalipokuwa tumenenda kumuaulia Zaynabu nadhiri. Tukingia kwa Shehke nako haifai kutolewa zipokeo tukapija wake hoya mashua zot'e zalizama, tukilinda wake hoya, ni yeo mashua zimedondomea, ehe tena haya kukisomewa Maulidi. Salama salama wat'u wakavuka salama. Ukenenda kubaua kulikukitokea mayongoo pete wakampambania mt'u. Tasubutu kubaua ? Kwalina karama kwa kweli, kama hiyao tumekwenda siku moya twalikwenda kuwaulia nadhiri hapo, alfajiri hakuya adhini wa mara husikia mt'u yuu la mnga, katoka bin Athmani kenda p'wani katawadha karudi alfajiri. Swala ! swala ! swala ! na tumetoka hapa saa nane usiku twalitukuzie ziatu za matepe na t'aa tukaisahau hapa ya simu tukishuka tena bin Athmani akavunda k'uni kukawaswa moto palee na palee kukawa marurumbi ya moto...eh, t'aa ilikuwa ni moya ikenda kulee msikitini.

Matondoni : transcript of hadithi Mbaraka Msuri by Mzee Fadhili Muhammed Shee

Mbaraka Msuri alikwenda Amu alikuwa ni ndhee wa Matondoni na Shahibu Msuri ni kina Ali Hani Mwanakombo Msuri. Mwanakombo Msuri alindhaa Mwarabu Hamisi babake ndhee mwarabu. Shahibu Msuri alik'eti nyumba ya p'wani ya kwa Hadhija Tota. Na huyu Mbaraka alikuwa na farasi wake. Basi dasturi ya wafalume watokapo kilikuwa na baraza. Sasa hakuna baraza. Baraza ya wat'u wawili ? Baraza ni kulee hofisini bendera ipepeako. Alichenda kwenye baraza na rafiki yake. Kenda siku ya kwanda alipanda farasi na rafiki yake palee Amu. Si rafiki wa hiya kwa hiya, ni rafiki ampenda hana hiyana naye. Kenda mpaka kwake kifunga farasi wake. Sasa alopokwenda nneno wa kulee Amu maina yao hupotowana. Ni hao kina Mmadi Mawia babake ni Mawia hawaankuani Mmadi Mawia Bwawia, ni hao kina Athumani Mawia, Athumani Bi Mawia, ndio walokichankuana ndio lugha yao wenyewe. Alopochenda Mbaraka walee walikimwankua Bwa Baraka, na hapa hankuliwi Bwa Baraka ila Mbaraka Msuri. Eee, ulee bwana akiangalia hawa hunitukana kiswanaa. Yaule hankuana Bwawia babake hoyo Mmadi Mawia, hoyo Mawia. Sasa katika baraza hio luwali ni Mmadi Bisudi bibiye huyu Hamadi Sudi. Basi alopoangalia hawa hunipopotoa, Bwawia ? kantukana babake Madi Mawia. Walee nlugha yao huyu kaona mmatango huntkuana kamwankua hee Bwawia, naye ni jagina hoyo likawawasha. Bwakari, Bwafadhi ikawa ni kupopotoana maina. Huyu Mbaraka aliandama kilima kilee likawakera likawa ni kishungi kikuu. Alopoondoka ulee katika baraza palee, yalingia huku na kuntoka kwa huku ili kuwajibu lugha ilee Bwawia, Bwasudi wakaona utungu. Wakanena, sasa ulee ni kumpija dhikanya, ni kunshika tukampija dhikanya tukamuua. Kadhengewa chondoka barazani kapekewa asikari,

lakini alopoondoka asiwe ni mwenye kuk'eti kapanda farasi ulee kamuaga rafiki yake kenda dhake. Ulee rafiki kasikia hukumu hini kuwa hudhengewa ulee kupijwa dhikanya. Alopokwenda mara yapili kifunga farasi ulee, ulee ni rafiki yake kamwambia, bwana mimi napenda neno moya: usiye katika baraza ya kina Mawia na kina Sudi sababu siku ilee walokwenda walee hankuana Bwawia, Bwasudi, nawe wakakwankua Bwa Baraka nawe likakuudhi Bwana Mbaraka, ukaankua Bwawia Bwasudi, ili hoyo luwali. Sasa alimwambia ulee rafiki yao hudhengewa kwa dhitimbi kuuwawa usiye tena katika baraza, kamwambia nakupenda. Kaya dhake ulee na p'unda wake asende tena, kiya ulee katambua chondoka kulee baradhani. Unaye mwane hankuliwa Bwana Famau, Bwana Famau wa Mbaraka na nkwewe Mumadi wa Bwana Famau, babake huyu Adinani bibiye hawa kina Madi Adinani, bibiyao alinafia aliodhee kwa mwane nao ni wamoya. Kamwambia, mwanangu Bwana Famau toka mui, na wewe nkwewa wangu Mumadi kwa hisani yako na yangu napenda dhijana dhangu utoke nao mui. Niatani niuwawe pweke yangu sitaki kusaidiwa, kawambia maana yake mimi hudhengewa kuuwawa na wewe ni nkwewa wangu, unionapo mimi utakwenda kumpija kuwali utantinda luwali, na nyumba itakuwa haina mt'u ni wanawake, wanawake hawana shauri. Nyumba nikuweko mwanamume, heri musalimike nyinyi nende waniuwe mimi. Wakaidha walee mwana na ulee nkwewe akamwambia, la, endani ufuatani na nyinyi wat'u wa Matondoni hapa sitaki kusaidiwa na nt'u mmoya. Niyapo kuwawa sitaki kungiliwa na nt'u mmoya ndani ya mui, maanaye keshole mutanena Mbaraka Nsuri metuua na sisi. Mimi nimentoa nkwewa wangu, kijana changu nde ya mui, na hapa (Matondoni) walikuweko wat'u wa afia lakini watawaka kwa bunduki ? afia dhao. Basi sitaki kungiliwa. Sasa kawa huindwa tu, baradha ya kwanda hakwenda, ya pili, ya tatu, walee wachangalia huyu bwana ulee hayi tena. Baradha hendi tena metimidha mara t'atu, huyu metambua yalee ya maina kupopotoana naye mejibu ni tango, meona ntango, nasi hudhengea kunshika hapa kumfunga, huyu mepata nt'u memwambia. Sasa Sudi babake Madi Bisudi, bibiye hawa kina Hamadi kamwambia, sasa hukutoa viboroto. Askari walikuwa wakiarabu sio hawa makavirondo weusi walikuwa wakiarabu hapo. Kawaambia nikwenda kumwandamia hoko alioko wakatoka asikari dhaidi mia, mume bunduki, mume bunduki, ee, utawala wewe bunduki hidho ? Ilee simbo utapata wawili uwak'ukute ni hapa na palee, simbo itainuka au panga ? Sasa wat'u wamefanya hamu kusikia bwana hudhengewa. Sasa saa ilee walokuya kwa maguu hawakuya hata kwa stima walikuya ni faragha ili asisikie mvumo, walikuya kwa huku kwa nlango, wangine si kutembea kwa maporini ? wakaona askari hupanda pamoya na ulee luwali kapija mbio, kipija mbio vuuuu..mpaka muini, kawambia napone Mbaraka Nsuri si asikari medhowatukua Sudi. Kula mmoya bunduki, tauwawa na Mbaraka Nsuri, katoka nt'u kenda kampa habari Mbaraka kamwambia, Bwana, pona, Sudi uyao na asikari dhaidi mia, kula mmoya bunduki, uyao kupijwa wewe. Eee ?

Kamwambia hao hapo nsikitini ulikuwa uikswaliwa. Basi ulee mwenye kumpa khabari hutetema taka kwenda nyumbani, kamwambia, enda dhako ukaisite. Kijana ulee kitoka chenda dhake lakini kila amuonao humpa habari, askari wamekuya kumuua Mbaraka. Kula asikiao kafunga nlango, kukafungwa milango mui ndhima. Mwalimu Sheikh Madi Fadhili hutwambia ni jirani na Hadhija Tota, hunena kaya kaukadha nlango. Muini kumelaliwa saa nne dha ntana. Wat'u wengedhe lakini kula nt'u mekucha baa. Basi sasa wakak'eti nsikitini askari wot'e na Sudi. Hapa (Matondoni) ulee Sudi hamuisi, amuyuao nt'u mbibiye hawa. Si hatumuisi babake Ali Gosho hoyo ankuao nyanyi hoyo, ndie amuyuao ni mwarabu mwende ulee Sudi naye uko hapa umuodhee Babu Hadi nduuye Madi Hadi. Akak'eti naye mekuya hapa, nsikiti ukayawa tele kwa bunduki. Kisa kufungwa milango ulee kawa hamuoni nt'u. Ulee Mbaraka unaye ntwana hankua Mirambo, uko nde ya mui minadhini hoko haisi habari ya mui. Akiya huona kufundiwefundiwe milango ntanaa, aaaa huwadha hamuoni hata nt'u ngaa tamwambia niye. Hunena nendao hata k'ipekea mato nsikitini huona ni askari wakiarabu walele kumoya. Palee mekucha ntwana hana nafasi. Bibi yake huyu babake Ali Bini Ayasi akamwankua Sudi, latika, latika, latika. Akamwambia, ukiwa wantaka Mbaraka Nsuri ntumwake Mirambo ulee ndie amuyuao Mbaraka Nsuri maana yake wao wangaya hawaisi ilee nyumba ya Mbaraka Nsuri, akamwambia, ukiwa wantaka Mbaraka Nsuri Mirambo lilee ntumwake. Kamwambia, ni ntumwake ? Kamwambia, ndie ulee ndie amuyuao. Askari, kamata ulee upesi, wakainuka askari sita sabaa hiyao na bunduki. Ntwana ulee medangana metatana kisikilia dhit'u dha bakuwe, wakamwambia, ngoja, ngoja, ni nni ? Wakamwambia, wewe nyanyi ? Nsikitini kuyewe tele bunduki na askari. Hunena iye ? ulee Mirambo kawaulidha, wakamwambia akuulidhao ni Bwana Luwali ulee, si tumeambiwa kukukamata tu. Hucha kwenenda bunduki dhilalie kumoya hata chenda Bini Ayasi babao kina Ali Gosho, kamwambia hoyo ndie amuyuao Mbaraka Nsuri, ntumwake hoyo. **Askari** wakamwabia, wewe ndoo mbee huku, chenda ulee ntwana udengene utetene nyama dha muili huntetema. Kamwambia, nip'a Mbaraka Nsuri aliopo t'akupa askari uwapeke. Ah, simuisi, simuisi. Alimwambia, sikiza we, ntoe Mbaraka Nsuri aliopo askari wakuandame. Simuisi. Aliwambia, askari mpije bunduki mpije mbwa hoyo..aaa, bunduki dhilee kula mmoya yake, ntwana changalia mauti haya mbeembee, ukishikwa nti nkavu. Kamwambia, ngoja, k'awaonye, ngoja, amuyua uko huku. Tena kiwatukua chenda nyumbani uko chumbani nyumba hini ya Bini Omari na dirisha lilee lekelee nsikitini wa Juma, ndio alouwana sefu ilee ilee. Sasa hiyao kuk'eti katika kiwambaa kilee kit'anda palee karibu na nlango pana kilili uk'etidhie, lakini na upanga wake ili atiao guu apate kwa nkono wake nt'u huuwawa naye ampata ? Nlango ulee wadhi. Asa hata kama aliufunga wangaliutekua, ni nguvu hidho dha kupija mateke ti, na ulee wachumba upande mmoya wadhi, yeye uk'etidhie penye ulee wadhi hungoja atiao guu.

Saa ilee wakiya Sudi kawambia, idhungukeni nyumba yot'e. Ngao dhot'e bunduki nkononi, imeshikwa nyumba mbee na nyuma. Wamekwenda hawamuisi kama wamuyua nkwenenda tu dirishani tu palee, lakini wakasimama tu tanabuhi hio isiwangie. Ngia ngia ti uko huku. Wafuetene kama askari watatu wakisimama wachangalia ni upanga nkononi ulee nae wakiangalia ni nt'u wa tani. Wakamwambia, tumetumwa sisi kufanya nni, yeye hamu yake iko kidhingitini humwangalia ulee atakao kutia guu. Tumetumwa na luwali Sudi kukupija dhikanya, maana ye hakuwambia mpijeni aliwambia mpijeni dhikanya, munietee huku nsikitini tupate kuntukua. Aliwambia, munipije dhikanya nyi ? wakamwambia, eee. Akawambia, muungwana hapijwi dhikanya. Dhikanya dhangu mimi ni sanda na kiunda kutukuliwa kudhikwa. Nyinyi mbwa dhikuyu munipije dhikanya mumpekee Sudi ? Hata mara moya. Na yeye Sudi tuonyane ume mimi na yeye, ninkadhe nimfinye mavi yantoke hapa, sikutukua askari. Na yeye tuanyakuane ayuwe alio mume utukudhie bunduki dhienee kwani huwana jihada ? Kantukueni yeye. Aaa, tutakushika, askari ni hayo. Aliwambia, haya ndooni munishike. Kitia guu wawili meutoa kipija dhwaruba ya upanga mewak'ata mikono wawili. Ulee abakieo watatu meuk'a hapa hata kulee. Walee midamu huwatoka. Wakitoka nnde, ' askari watende. Eee, mbona hamukunshika ? Wakawambia, nyinyi muna wadhimu ? Waliwambia, hashikiki. Kwa nni ? Wakawambia, asad, simba, simba, ukisimama katika kidhingiti hurusha upanga kakuk'ata, simba. Waliwambia, hashikiki, nkuwata ruhu. Basi hawa walioko nnde wakaidhi, waliwambia, hashikiki ? Wakawambia, asad, simba, Mbaraka simba, ila uwate ruhu yako pale pale. Hawa walioko nnde wakofundi dhaidi walimwambia, dhurub dhurub, mpijeni bunduki tashika hashikiki ? Wachangalia lilee dirisha huona kwa kimo walee askari hawakuwa na tanabuhi wangilikuwa wamentoa kitambo. Uko wapi ? Kamwambia, hapo penye dirisha. Kisimama kwenye dirisha Mbaraka Nsuri ulee uk'etidhie. Ni hayo ntanda nshinde hana shauri. Bunduki mia utawana iye ? Wakatoka wat'u wa mui ndhima hawawani. Simbo itawana wa ? Takupija hapa hata kulee utakuwa ukitataa. Dhurub. Walee wakamwambia, uko hapo dirishani uchekedha unae. Sasa walee huona dirisha lilee hukoma kifuani. Sasa ulee bwana hana shauri. Aliwambia, dhurub. Aliinyosha katika t'undu ya dirisha huona kilee kimo, alinlenga tu. Kinlenga kimpija na bunduki haina matedho. Kiuk'a kitaataa, pupu pupu pupu. Wakimwangalia mekwisa mekwisa kufa. Alopokwisa kufa ulee Sudi metambua palee nsikitini na walee askari walioko kuwa hawakumpija dhikanya hawakumuwedha, akisikia bunduki kanena wameua. Nami sikuwatuma kumuua, naliwambia mpijeni dhikanya ulee aliwambia, mimi sipijwi dhikanya kupekwa kwa Sudi angawa luwali. Dhikanya dhangu hupijwa nifapo katika sanda, lakini Sudi hanipati na yeye tupambane. Tuonyeshane Usudi wake nami nimuonye Mbaraka wangu, una afia mmipanga ilee ya kiswahili minene si p'anga hidhi dha kutetema, ni ilee minyangarika kana wegu. Chenda. Wapi Mbaraka ? Wapi

Mbaraka Nsuri ? Wakamwambia, tumemuua. Kwa sababu naliwatuma mpijeni mumue ? Naliwambia mpijeni dhikanya, munietee, sikuwapa ruhusa kumpija bunduki. Wakamwambia, bwana luwali huisi habari ya hoyo wewe. Walimwambia, tumekwenda kumpija dhikanya uko nlangoni na panga lake nene nae una na afia na nlango ni mmoya. Ufungudhiwe upande mmoya na yeye ekedhee nlangoni una hadhwari. Tuchenda tukamwambia tumetumwa na bwana Sudi luwali kukupija dhikanya na ametujibu sisi hutwambia mungwana hapijwi dhikanya ila sanda na kiunda na yeye. Basi tumengia sisi tukitia mateke uweshee upanga wake tukitia maguu metupija upanga askari wawili, mek'ata mikono, mmipanga ilee ya kiswahili kama wengo mipini. Tumetoka nnde wamekwenda namba ingine, watatu kusimama ili kama sisi mmagoigoi, wachenda nao wamepijwa hawakufa tu lakini dhimewak'ata mikono. Sasa tumedhopoona palee wa pili wamedhopok'atwa walee wametupa ruhusa. Twaliwambia, Asad, Asad, simba, hashikiki, Mbaraka simba. Walitwambia, dhurub. Ilee dhurub, bwana luwali, tumesimama dirishani tumemwekedha bunduki tumemuua. Sudi kawambia, sikuwambia muueni. Walimwambia, hashikiki yeye alokuwa hutuua tumeichea ruhu dhetu. Kufundiwe milango mui ndhima hakuna fahali aatamao. Mui kama usiku saa' nane hawakulala walonekanwa walee askari wayao ikaenea habari. Wat'u wa Matondoni kwalikuwa na wat'u wenye afia wakanena ni hoyo Mbaraka Nsuri, na hio si akili waloidhua, ni kuutia moto mui ndhima, hio ni akili ? Sasa walee hawatakimbia mukiutia sio ? Sasa wakiona rurumbi watak'eti hasara si nyinyi wenye majumba ? na ilee sirikali ikiwataka itawakosa ? Si bunduki dhitaenea usiku hakingia mutakimbia wa ? Basi sasa ulee Sudi akawambia askari t'antukua huyu maiti, huyu Bwanakombo wa isufu ni undugu babao hawa kina.........katika kaburi. Basi t'atoka mimi na Mwarabu wa Helefu k'aombe kwa luwali Bwana Sudi ili huyu Bwanakai kuwa huyu bwana wetu nduyetu twatie wenyewe tudhike kwa utukufu wako na edhi yako. Umetaka kumuua Mbaraka Nsuri umedhie lakini kudhika bwana tafadhwali, twatie wenyewe, mimi mmedhokuya ni nduyake hio Mbaraka Nsuri. Basi twatie tudhike wenyewe. Huyu naomba kwa utukufu wako wa chec na kimo sirikali yako na yetu utwatie wenyewe kama kuntukua sipitali nkufumwa tu. Niwaatie ? Sudi huwambia tuwatie nduyangu mimi tafadhwali. Eee, asa twaliambiwa ulee akushindao si mwendo asa nae awedha kumuua hapa hapa askari mia wampije bunduki hakuwi lolot'e, hayo nda akhira. Akamwambia, basi haya t'aenenda dhangu, kwaheri. Kawambia askari, haya twendeni dhetuni. Alimwambia, lakini Bwanakai nt'u wenu hatukuntukua, meuwawa tu uko koko nyumbani. Haya bwana, basi hunyenyekea humuinami ni luwali na maasikari nanna hio. Hakuna ushujaa hapo wala uume, kwaheri. Kamwambia, kwaheri, bwana, santa, santa. Hakuna alotoka mmoya kumwandama Bwanakai kwenda kuntaka kufundiwe milango kot'e, hakuna mmoya, Sheikh Mmadi Fadhili hunambia hakuna nyumba nlango wadhi hata

mmoya, nae nkulee uukedhe wake nlango kwandani nkana barani hakuna yoyot'e, na Mbaraka Nsuri si kulee utapwani, kwa shahibu, nyumba yak ni hini hini ya p'wani kwa Hadhija Tota ndio aloket'i. Kaambiwa alik'etidhie palee penye dirisha leekedheeo nsikiti ndipo alopoekedhwa. Nalo jumba kuu hapo, na hao kina Mwarabu Hamisi mamao alinalo jumba nao wakafa wao walinalo jumba la mawe mawe hiyao, nda hoyo Bamu wa Nsuri nduye Mbaraka Nsuri mamake Umari wa Bwana Hamisi. Nyumba yake ni hini wamodhowaka hawa huyu Atika uwanda wao. Wakafa wot'e huo na uwanda ndatoka hao babayao.

Transcript of ngano recorded by Mwana Fatuma Nyenye

Aliweko tajiri mmoya, tajiri hoyo kaoa nke. Alipooa nke akadhaa kijana mwanamume kak'eti kijana chake hata kikua. Akipata nyaka sabaa katenda mimba tena ya pili. Akadhaa kijana tena wa kiume sasa lakini ulee wa kwanda medhie kuwa nkuu. Basi kak'eti nao tajiri kak'eti nao mpaka ulee sasa wa kwanda mekuwa mpevu kaodhwa nke. Kenda kak'eti na nke wake. Kisa kupoa nke wake naye nke wake katenda mimba kadhaa. Ulee sasa nduyake tena mekuwa ni barobaro. Wakak'eti hata mara babao ulee kashikwa na maradhi kishikwa na maradhi kawa hata dhiyakanthakilisha. Alipoona thakili kamwankua mfalme, akamwambia, mfalme mimi siwedhi na mwanangu huyu nimedhie kumuodha na huyu ni ntoto, basi nami nimohufa. Basi haba haba wanangu wawili, na haswa huyu ntoto. Basi akafa tajiri ulee, alipokwisa kufa kadhikwa, kuk'etiwa matanga kukahaliliwa kukesa mambo yot'e. Sasa kisa kufa mwananke sikualikwa eda ? Basi mwananke ulee kaalikwa eda siku ya kwanda, ya pili, ya tatu, kipata siku ya nne ulee kijana wa kiume wa kwanda mekuwa huntoa, humwambia, toka wende dhako, sitaki kukuona hapa kwangu, uk'etidhie hapa huna ufanyalo hula tu, basi toka. Ulee nke wake humwambia, haifai hiyao, asa kiwa ni mali haya si yenu nyut'e, kula mmoya hana haki yake ? na tena hayakuawanywa. Ulee mumewe humwambia, sitaki mwenyewe natoke ende dhake. Sasa ulee mwananke umuweshee humpa chakula kwa siri, siku ya kwanda, ya pili, hata ya tatu ulee kijana alipotoka kadhini hoko hafisini kaya kandirika ulee nduye nyumbani, kaya kandirika ulee mwananke humpa chakula kanrukia ulee mwananke kamwambia, mimi simekwambia usimpe chakula huyu ? we husikii humpa chakula tu. Basi ulee kijana akatoka kakimbia. Alopokimbia sasa kawa tena hana pakwenda mekuwa hulala baradhi hini kilala baradha hini kwao hasubutu kwenda, kawa kijana husikitika mekuwa huomba palee chondoka palee. Kijana cha kitajiri mekuwa huntambui mekuwa maskini. Sasa kijana kak'eti kiasi cha siku k'umi medhiekuwa maladhi yake, ni baradhani tu. Siku moya ulee

kijana uk'etidhie baradhani usiku yapata kama saa sabaa hiyao, katiti aone wat'u hupita. Kijana kivua mato kaona nlolongo wa wat'u , kaya kawandama, kawandama pupupupu mpaka wakasikilia jumba moya kuu, alopokwenda kalama ni wadhi. Walee wakajep'a nae kijana ulee kajep'a. Walee lakini hawankuntaa mali, sasa walopomalidha wakarudi. Kalama wana jumba ndani ya mwitu ndiko waekapo dhile dhit'u dhao. Wakenenda mpaka ndani, ulee kijana nae umo. Basi waloposikilia nlango ufundiwe ulee, kasimama ulee amiri wao kanena Patis, kinena Patis, ulee nlango hufunguka. Walopofunguka wakangia na dhile dhit'u dha kujep'a wakadhiweka, nae ulee kijana kangia nae kaweka dhake. Alopokwisa kashika ndia kenda dhake. Basi imekuwa ni kadhi tena. Mekuwa ulee kijana kula siku huwaandama wakijep'a wachenda wakitia mali. Hata ulee kijana kitia akili kanena ruhuni mwake, sasa wakiwa hawa hujep'a usiku mimi t'akwenda kuwajep'ea ntana. Kama sura waswahili wanenao yakuwa, nyang'anya hanyang'anyi, ila nae hunyang'anywa. Basi ulee kijana kawa ni mwenye kwenda ntana, kenenda kisimama kanena neno lile lile wanenalo wedhi wa usiku, kanena, Patis. Nlango ukafunguka ulee kangia nae kajep'a, katukua mali kenda kafukua tobwe lake nae kawa hutia mali yake. Katia masanduku ya. dhahabu, katia masanduku, katia masanduku, ikawa ndio kadhi yake sasa. Walee wangine hawayatambua tu, kawa yeye usiku henda kujep'a na wale wende usiku henda kujep'a ye pwekee. Sasa walee jamaa dhake huona mali yao katika ilee nyumba yamepungua lakini hawaneni. Kijana kendeleya na mwendo hoo mpaka kaona, ehe, sasa nimepata mapesa mangi, kantuma nt'u ndhima, kamwambia, ninunulia nami nyumba. Kannunulia nyumba ya dari na dhisima ndani na kula kit'u shilingi t'uu, kankadhibisha mwenyewe. Nduye kulee una duka hayaisi mambo hayo kabisa. Kisa kununua nyumba kenda kamwambia ulee nt'u alontuma nyumba kamwambia, nataka ukaninunulie dhombo dha nyumba, dhitanda, magodoro na kula kit'u, dhot'e unitilie nyumbani mapesa mimi t'akupa. Sasa humpa pesa ulee, mekuwa ni rafiki yake, mekuwa ulee kijana humpa ulee rafiki yake pesa, ulee kitia nyumbani dhombo, kaipamba nyumba kwa kula chombo kilioko duniani. Mara siku moya katoka ndak'u kenda kamwambia nduye kamwambia, nduyo ununudhie dari kuu metia dhombo, hushinda hio nyumba na duka lako, kamwambia, nduyangu ? ulee kamwambia, nduyako. Ni ye nduyangu kununua nyumba ? nae ni maskini, chakula chake hana na huku kwangu mimi nimentoa. Ulee kamwambia, kwani ulee nae si wa mungu, kwani hata unene ni maskini ? Wat'u wakawa humwambia, nduyako menunua nyumba, lakini asiamini, kipata nt'u nngine siku ya pili, kimwambia yale yale, asiamini, siku ya tatu, siku ya nne alintuma mwane, kamwambia, ndoo ukanankulie. Kijana ulee katoka vuuuu mpaka baradhani ulee nduyake babake ulele, kenda kamwambia hankuliwa na babangu, ulee kashtuka kamwambia, babako ? ulee kijana kamwambia, babangu ndie akwankuao.

Ulee kafikiri moyoni kanena, hatuisi kunani,**huyu** menitoa kwake kisa yao huwa iye anitaka, labuda mepata nt'u memwambia sina shaka. Ulee kijana humwambia, baba menena upesi. Ulee kamfuata nyuma, wachenda guu kwa guu mpaka kwa nduye, kenda nduye ulee uko dukani uk'etidhie kamwambia, nina madhungundho yako nataka kukweledha, lakini nataka uye saa nne dha usiku. Kijana ulee kishika ndia chenda dhake. Saa nne ulee kijana mekuya, una hamu, kiya kamwambia, haya nip'a habari, nimesikia umenunua nyumba, senti hidho umedhipata wapi ? Ulee kamwambia, medhonip'a ni mngu. Ulee kamwambia, la, la, la, sitaki maneno nataka unambie umedhipata wa ? au kama hutonambia kitwa chako ni halali yangu au changu ni halali yako. Kijana kamwandia tena kamwambia, pulika kwa udhuri sana, tena kamuhadithia kamwambia, uliponitoa kwako nik'ilala baradhani. Siku moya k'awaona wat'u hupita k'awaandama, k'iwaandama kalama ni wedhi henda kujep'a, wachenda kujep'a nami nalichenda. Wakiya nadho dhile dhit'u wanalo jumba lao ndani ya mwitu, ndipo waekapo, wakiya nami nalikiweka. Basi tukawa hujep'a tukipeka jumbani wala walee wedhi hawakuniona hata siku moya, na kulee kwenye jumba wasikiliapo hunena Patis, nlango hufunguka wakangia. Mara akili ikaningia k'anena hawa hujep'a usiku nami t'akwenda kuwajep'ea wao ntana. Basi k'awa nami hujep'a k'ikusanya katika tobwe langu hoko ndani ya mwitu, ndio haya mapesa nimedhopatia nyumba. Ulee nduye kamwambia, haya nimekusikia maneno yako, sasa nataka ukanionyeshe hapo mahali hoko ujep'ako wewe ntana nami nataka kwenda kujep'a. Ulee nduye kamwambia, ngoja t'akuonyesha, basi asubuhi, kamwabia, haya. Kijana ulee kaket'i hata asubuhi kainwea shai yake kikoma katiti mekuya kijana kumwankua. Ulee kijana kenda kwa nduye chenda kamwambia, haya nimekuya. Nduye ulee kanruk'ia kwa ukali kamwambia, twende kanionyesha palee mahali. Nduye ulee kamwambia, lakini uyue mimi sitokaribia nlangoni t'akuonyesha tu kwa mbali. Wachenda mpaka karibu na ilee nyumba, nduye kamwambia, haya, nlango ni na maneno nimekwambia ya kunena, mimi nendao dhangu. Kirudi muini ulee kenda kisimama nlangoni, kisimama kanena nlango Patis, nlango ukafunguka, kingia ndani, Patis, nlango ukafungika. Basi tena kikusanya masanduku ya mapesa kikusanya nlangoni kikusanya kikusanya. Sasa taka kufungua nlango atoke nayo masanduku, kitaka kukumbuka maneno yalee hawedhi, **medhie** kuyasahau. 'Tokis', kinya nlango, 'Siisi', kinya nlango, 'Sitaki', nlango kinya. Kapija mayoe ataka kulitanka neno la Patis, lakini wapi p'u hawedhi. Hapa palikuwa ni saa t'ano dha ntana, kasimama kutwa mpaka usiku. Tena dhimekuwa ni t'aimu dha wenyewe kwenenda. Kijana ulee nduye ulele baradhani, katiti walee hupita, kanena, yeo mimi siwaandami, medhie kuyua kuwa ulee nduye mefungika kulee. Walee wakapita wakisikilia wenyewe wakanena Patis. Patis nlango tayari umefunguka. Ukifunguka

kijana usimeme nlangoni. Eeee, hiyao sisi mapesa yetu hupungua kalama ni wewe huya huku ukatuwin<u>d</u>a hatuko n<u>t</u>ana ukatujep'ea ? Basi yeo u<u>t</u>aona cha ntema k'uni. Wakaweka mali yao wakampija mpaka wakamuua. Wakikoma wakan<u>t</u>ururua mpaka si<u>t</u>ani. Sasa huyu nduye kalala mpaka asubuhi, mara asubuhi umuonee nke wa nduyake kamwambia, yana mume<u>t</u>oka pamoya na nduyo, mbona yeye sasa hayarudi ? Ulee nduye mumewe humwambia, Eeee, hakurudi ? Basi ngoja k'amwangalie. Kenda kimwangalia ufie, kirudi kimwambia nke wake kamwambia, mumeo medhie kufa. Sasa ? Sasa niku<u>t</u>ukua san<u>d</u>a tukenda tukandhika na wat'u. Basi <u>t</u>ena ika<u>t</u>ukuliwa san<u>d</u>a na wat'u kenda kadhikwa hoko hoko. Huyu nduye kais<u>t</u>warehea yeye kenda dhake.

Mwani: a story

Ikiwapo inti moja, inti-yo akiwapo mfalme, lakini mfalme wenyewe sió binádamu, alikuwa ndi jini. Ntimwi-yo kèekala na raia zake, raia zake zikiwa nyama. Akiikala, mwaka mmoja atowa maji. Akitowa maji kàlavya amri, kàmba: "usimbiwé nrimbu !" akimwita waziri, akiibiya umambi, waziri akibiya umambi, waaja nyama pia. Ila sungula aajire. Wakisimba nrimbu, "Sungula kàwa ndepi ?", kàmba: "Sungula aapo". Ukisimbiwa nrimbu, wiisa, neema peekala. Mfalme jini kawaámbira kamba: "Sungula musimwase kuteka maji, na akija kuteka maji, munkore !" Akitwariwa nembo, akituriwa kwikárira maji. Akituriwa kwikárira maji, sungula inkola nyota; n nyumba mwake amuná maji. Kàtwala malamba, akitobola, akipangira, kuno kumi, na kuno akipangira kumi. Wakati wa kuuka, kèengira kusówera: "Gungundú, gungundú ! ninsíngane nzee nembo, nimponde-pondenge ! aniíjiwe ali yangu ! gungundú, gungundú ! ninsíngane nzee fisi ! nimponde-pondenge ! aniíjiwe ali yangu ! gungundú, gungundú !"

Nembo kèekala kàfikiri: "Omi nìwa nkulu, nikóopesa dunia nzima-yi ! eyu munu-yu aja kuniponda-yu, kuniponda munu kamba-mi ! í ! aatoweke !" Nembo akituwa, akuuka vyake. Sungula akija, akiteka maji, akuuka vyake.

Mfalme akaamba: "Mwaja ?" Kàmba: "Sungula ! eyu sió sungula, ciija-co kikulu ! Omi, nìtuwa, sikidiri kuikala; tena munu-yo mwingi !" Mfalme jini kàmba: "Kùwa nlongo, tena aufai, fwadari timpéreke nyati !" Akiperekiwa nyati kwikárira maji. Subuu sungula kàlawa na malamba ake ishirini nyuma, ishirini mbere. Akuuka karibu, akifika pa nrimbu, kàanza kazi yake noire-ire: "Gungundú, gungundú ! ninsíngane nyati ! nimponde-ponde ! gungundú, gungundú ! ninsíngane faru ! nimponde-ponde !" Nyati eemirire, akisikiriza kamba eyo aja-yo kinu; akituwa, akuuka vyake. Kòoka kure, kàfika, kàpiriguntari: "Kinani ?" Kàmba: "Sikidiri kwikala ku nrimbu; eyo akúulaya wanu, tena ámiza wanu, sió sungula !" Sungula kàja, kàteka maji, kòoka vyake.

Hata suku moja, kàja ambe, kàmba: "Mfalme, niperekee-mi ! nuuké kuńkola sungula." Mfalme kàmba: "Kùwa tolu sana ; kàsokerera nembo, munu nkulu wawenye, kàsokerera nyati, asemiwa nguvu. Uuké uwe, uwe ndi nani ? Eyo munu-yo munu !" Ambe akivuta, akikala kure.

Kàmba: "Timpéreke mera !" Akilawa mera, akuuka kwikárira maji. Sungula subuu kàlawa na malamba hamsini: "Gungundú, gungundú ! ninsíngane mera ; nimbonde-bonde ! gungundú, gungundú ! ninsíngane simba, nimponde-ponde !" Mera kufíkiri, roo aimwikárire pansi, kàtuwa. Sungula kàaja pa nrimbu, kàteka maji, kàlawa, kòoka vyake. Akiperekiwa simba, akuuka kwikárira maji. Sungula kàaja nao malamba mia; nare malamba wakati weemba akitikinya, aankuvuma: "Gúngundungu, gúngundungu, gúngundungu !" Kèengira

kwimba: "Gungundú, gungundú ! ninsíngane simba, nimbonde-bonde ! gungundú, gungundú ! ninsíngane simba, nimbonde-bonde ! "Simba kusíkiriza, kàmba: "Epa apeekárika !" Kàtuwa, kòoka vyake; sungula kàaja, kàteka maji, kòoka vyake.

Ambe kòoka tena ka mfalme: "Mfalme, nipereké omii ! munu-yo niñkola !" Akilawa mfalume: "Kamba aunkorire ?" Kàmba: "Kamba sinkorire, njo unuúlaye !" Wanu wakilawa, kàmba: "Mfalume, aumpereka ?" Ntimwi kàmba: "Njo kuno !" Kàmba: "Ukúuka kuñkòla-ja ?" Kàmba: "Omi, vya-nisaka, mutwaré sera, munipake pa minyongo." Wanu wakitwala sera, wakimpaka ambe ku minyongo kuno, pii ! Ambe akuuka íréé...mpaka m maji mure. Akiritosa.

Subuu sungula kàlawa, akilawa kèemba nyimbo yake noire-ire: "Gungundú, gungundú ! ninsíngane ambe, nimponde-ponde." Kèemba ire, mpaka ásokera. Ambe asilawe. Sungula akisikiriza kamba emu maji-mu amuná munu. Akitwala lukasi, akiteka maji, akinywa. Ásaka kupéreka tena kuteka, lukasi rikòla upula ure. Sungula kàmba: "Paa ! como aunaaca kwanja !?" Kàmwefya nyate; kumwefya nyate, mulu upara pa minyongo nópare. Sungula kambà: "Nikwefya latuma." Kumwefya latuma, nae kàpara nópare. Akeefya nkono wa sonto, nkono sonto nae kàpara nópare. Akeefya nkono nriro, kàpara nópare. Kàɓaki nóvire. Ambe kèengira kuñyángula: "Naangupireni, naangupireni !" Wakija wanu pare, wakinkola sungula, wakuuka nao mpaka ka mfalme.

Ambe akipata kikombe: ikitendiwa ngoma, ikiviniwa sherehe, ulu sana. Sambi, ámuri ya mfalme ndi ní ? Yaambiwa kwanza: "sungula afungiwé ! Afungiriwé pa jua pare !" Akilawa sungula: "Omi, mfalme, únifunga na nzizi usaka kuwa wonse, nítupula, nikuuka vyangu. Ila unifunge na nlala mwisi, tena unaánike pa jua-po, nipaté kutubu !" Wanu wakisinja milala miwisi, wakija, wakimfunga sungula, wakintula pa jua. Na ṇlala, kamba vya-mwijiwa desturi yake, ukiwa mwisi, úrimba, ukipata jua, ukuumília, úrera. Kweli kwelini, sungula wakimwefya pa jua, mfalme akuuka vyake kwake, na wanu wakitawanyika. Pa-rikórera jua, nlala umília. Sungula kàlawa, kòoka vyake. Subuu pa-kucere, mfalme kòoka kuñnang'aniza sungula. Oláiwe ! aansingana, kàsingana kamba nupu ! Ndi mwisho wa adisi yangu.